



BODI YA KOROSHO TANZANIA



TANGAZO LA MAFUNZO YA UDHIBITI NA UHAKIKI UBORA WA KOROSHO GHAFI MSIMU WA MAUZO 2026/2027

Bodi ya Korosho Tanzania (CBT) inawataarifu wadau wa Tasnia ya Korosho nchini kuwa itaendesha **Mafunzo ya Udhibiti na Uhakiki wa Ubora wa Korosho Ghafi** kuanzia tarehe **07–12 Septemba 2026** katika **Chuo cha Mafunzo ya Kilimo Mtwara (MATI)**. Mafunzo haya yanatolewa kwa mujibu wa Sheria ya Korosho **Sura ya 203** Toleo la Mwaka **2023**.

Washiriki wanaolengwa

Mafunzo yanawahusu Wataalam wapya na wadau wote wanaotarajia kufanya kazi za uhakiki ubora wa korosho ghafi, wakiwemo Waendesha Ghala, Wanunuzi, Vyama vya Ushirika, Viwanda vya Kubangua Korosho, Maafisa Ugani, Maafisa Kilimo na wadau wengine wa Tasnia ya Korosho.

Vigezo vya Ushiriki

- ◆ Awe mdau wa Tasnia ya Korosho mwenye nia ya kupata mafunzo ya udhibiti ubora.
- ◆ Mwenye elimu ya Kilimo au taaluma zinazohusiana na kilimo atapewa kipaumbele.

Ada za Mafunzo

- ◆ Washiriki wapya: Sh. 500,000/=
- ◆ Wataalam wenye vyeti vya miaka iliyopita pamoja na Mameneja wa Maghala: Wahudhurie tarehe **12 Septemba 2026** kwa ajili ya maelekezo kuelekea msimu 2026/2027 kwa ada ya Sh. 100,000/=.

Malipo yatafanyika kupitia **Control Number** itakayotolewa na CBT. **Mwisho wa malipo ni tarehe 04 Septemba 2026 saa 10:30 jioni.**

Mawasiliano

Eng. Jamal Akida
Afisa Udhibiti Ubora – Bodi ya Korosho Tanzania
Simu: +255 676 576 591

ANGALIZO

Katika msimu wa mauzo 2026/2027, hakuna Mtaalam atakayeruhusiwa kufanya kazi za uhakiki ubora wa korosho ghafi katika Maghala ya Minada, Maghala ya Wanunuzi au Viwanda vya Kubangua Korosho bila kuwa na cheti halali kilichotolewa na Bodi ya Korosho Tanzania (CBT).

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU
BODI YA KOROSHO TANZANIA
August 2026.